

MAKAO MAKUU

Ghorofa ya 4, Jengo la LAPF, Barabara ya Makole
S.L.P. 2857, Dodoma, Tanzania

Simu: +255-26 2329002-3; Nukushi: +255-26 2329005

Barua pepe: info@ewura.go.tz

Tovuti: <http://www.ewura.go.tz>

TANGAZO KWA UMMA

MWITO WA MAONI YA WADAU KUHUSU MAOMBI YA MAREKEBISHO YA BEI ZA MAJI NA USAFI WA MAZINGIRA KUTOKA MAMLAKA YA MAJI SAFI NA USAFI WA MAZINGIRA YA BUKOBA (BUKOBA WSSA) KWA MWAKA 2018/19 – 2020/21

Maombi ya Mabadiliko ya Bei Na. TR-W-18-014

Mnamo tarehe 17 Agosti 2018 Mamlaka ya Udhhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA), ilipokea maombi yaliyokamilika kutoka Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira ya Bukoba (Bukoba WSSA) ya kutaka kurekebisha bei za huduma zake za maji safi kwa mwaka 2018/19 hadi 2020/21. Majedwali namba 1 hadi 5 hapa chini yanaonesha mchanganuo wa bei za sasa na bei zinazopendekezwa

Jedwali Na 1: Bei za Sasa na Zinazopendekezwa kwa Wateja Wenye Dira (Shilingi kwa Uniti moja ya ujazo)

Kundi la Wateja	Matumizi (Mita za Ujazo)	Bei ya sasa	Bei inayopendekezwa					
		2017/18	Mabadi liko (%)	2018/19	Mabadi liko (%)	2019/20	Mabadiliko (%)	2020/21
Majumbani	0-5	1,345	53%	2,053	13%	2,318	13%	2,620
	>5-10	1,370						
	Zaidi ya 10	1,395						
Taasisi	0-5	1,500	55%	2,328	13%	2,632	13%	2,975
	>5-10	1,545						
	Zaidi ya 10	1,620						
Biashara	0-5	1,510	55%	2,348	13%	2,653	13%	3,000
	>5-10	1,555						
	Zaidi ya 10	1,640						
Viwanda	0-5	1,810	54%	2,782	13%	3,142	13%	3,550
	>5-10	1,845						
	Zaidi ya 10	1,915						
Magati		750	100%	1,500	0%	1,500	0%	1,500

Jedwali Na.2: Ada ya Maunganisho ya Huduma ya Maji ya Sasa na Inayopendekezwa (Shilingi kwa Maunganisho)

Kundi la Wateja	Ada ya sasa	Ada inayopendekezwa		
	2017/18	2018/19	2019/20	2020/21
Wateja Wapya wote	20% ya gharama za maunganisho kama ilivyoelezwa katika Kifungu cha 24(4)-(7) cha Kanuni za Maji za Mwaka 2013	20% ya gharama za maunganisho kama ilivyoelezwa katika Kifungu cha 24(4)-(7) cha Kanuni za Maji za Mwaka 2013		

Jedwali Na.3: Ada za Sasa na Zinazopendekezwa za Kurejeshewa Huduma Baada ya Kukatiwa (Shilingi/Kurejeshewa huduma)

Kundi la Wateja	Ada ya sasa		Ada inayopendekezwa				
	2017/18	Mabadiliko (%)	2018/19	Mabadiliko (%)	2019/20	Mabadiliko (%)	2020/21
Majumbani	10,000	0%	10,000	0%	10,000	0%	10,000
Taasisi	20,000	0%	20,000	0%	20,000	0%	20,000
Biashara	30,000	0%	30,000	0%	30,000	0%	30,000
Viwanda	60,000	0%	60,000	0%	60,000	0%	60,000
Magati	0	-	0	-	0	-	0

Jedwali Na. 4: Tozo ya Sasa na Inayopendekezwa ya Kuondoa Majitaka kwa Wateja (Shilingi)

Kundi la Wateja	Tozo ya sasa		Tozo inayopendekezwa		
	2017/18	Mabadiliko (%)	2018/19	2019/20	2020/21
Wateja Wote	100,000	50	150,000		

Jedwali Na.5: Tozo ya Sasa na Inayopendekezwa ya Kumwaga Majitaka katika Bwawa la Mamlaka (Shilingi kwa gari)

Aina ya Gari	Tozo ya sasa		Tozo inayopendekezwa		
	2017/18	Mabadiliko (%)	2018/19	2019/20	2020/21
Magari Yote	7,000	0	7,000		

Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Bukoba imeeleza kuwa bei na tozo zinazopendekezwa zitaiwezesha mamlaka kulipa gharama za uendeshaji na matengenezo hususani gharama za umeme ambapo ruzuku ya Serikali ya asilimia 50 kwa gharama za umeme imeondolewa. Pia mamlaka imeeleza kuwa kuondolewa tozo ya huduma (service charge) kunaashiria kupungua kwa mapato ya mamlaka na kushindwa kulipa gharama za utoaji huduma, hivyo marekebisho ya bei ni muhimu.

Kwa mujibu wa kifungu Na. 19 (2) (b) cha Sheria Na. 414, kutakuwa na Mkutano wa Taftishi siku ya **Ijumaa, tarehe 21 Septemba 2018 katika Ukumbi wa Mikutano wa ELCT** uliopo Bukoba Mjini kuanzia saa **4:00 asubuhi**. Lengo la mkutano huo ni kwa ajili ya kupata maoni ya wadau ikiwa ni pamoja na Baraza la Ushauri la Serikali na Baraza la Ushauri la watumia Huduma zinazodhibitiwa na EWURA, wateja wa Mamlaka ya Maji Bukoba na wananchi wote kwa ujumla kuhusu uhalali wa bei zinazopendekezwa.

Wadau wanaopenda kutoa maoni kwa maandishi wanaombwa kufanya hivyo kwa kutuma maoni yao kwa Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa EWURA kwa anuani iliyoonesha hapo juu **ifikapo tarehe 27 Septemba 2018**. Maelezo zaidi yanaweza kupatikana katika ofisi za **EWURA KANDA YA ZIWA, GHOROFA YA NNE, JENGO LA PPF; BARABARA YA KENYATTA, MWANZA** au **OFISI ZA MAMLAKA YA MAJI SAFI NA USAFI WA MAZINGIRA BUKOBA**

Imetolewa na:
Kaimu Mkurugenzi Mkuu
Mamlaka ya Udhhibiti wa Huduma za Nishati na Maji
(EWURA)